



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO



Dar es Salaam
8 Mei, 2024

TANGAZO KWA UMMA

UTARATIBU WA UNUNUZI WA KAKAO MWAKA 2023/2024

Kwa mujibu wa sheria ya Usalama wa Chakula [sura 249] na marekebisho yake kuitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Na. 19 ya Mwaka 2009, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) imetoa mwongozo wa Biashara ya zao la kakao kwa kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala na kufanya mauzo kuitia mfumo wa mauzo wa kielektroniki wa soko la bidhaa tanzania (TMX).

Tarehe 9 Aprili 2024, kikao cha pili cha wadau wa zao la kakao kilifanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Lengo la kikao lilikuwa kuitia na kuthibitisha mwongozo huo. Katika mkutano huo, wajumbe walikubaliana na kuitisha miongozo huo na kuanza kutumika rasmi mwezi Mei 2024. Aidha, taasisi za COPRA, TCDC, WRRB, na TMX zimepanga kuendelea kutoa elimu kuhusu majukumu yao na uendeshaji wa mfumo mpya wa minada ya kakao kuitia TMX. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine unalenga kulinda ubora wa zao la kakao na kuongeza ushindani kuitia minada. Aidha, mwongozo huo unaelekeza utaratibu wa ununuzi na uuzaaji wa kakao kama ifuatavyo:-

- i. Mnunuzi wa Kakao anapaswa kufuata utaratibu wa uendeshaji wa minada ya Kakao ghafi mwaka 2024 kama zilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Biashara unaopatikana kwenye tovuti ya COPRA au kutumia: <https://www.copra.go.tz/publications/guidelines>.
- ii. Mnunuzi wa Kakao anapaswa kujisajili na COPRA kuitia kiunganishi <https://asds.kilimo.go.tz/login> au kuitia tovuti ya <https://www.copra.go.tz/>. **Usajili unatolewa bila malipo.**
- iii. Minada yote ya zao la kakao itafanyika kwa kutumia **mifumo ya kielektroniki inayoratibiwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX)**.
- iv. Cheti cha usafi wa mazao/mimea (phytosanitary certificates) kitatolewa kwa kakao itakayopitia mfumo huo.

- v. Kibali cha kusafirisha nje ya nchi kitatolewa kwa kakao uliopitia kwenye mfumo huo.
- vi. **Minada ya kakao itafanyika kila Jumatatu kupitia mfumo huo.**
- vii. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kutumia [+255 733 800200](tel:+255733800200) au registration@copra.go.tz

Tangazo hili limetolewa na:



Irene M. Mlola

MKURUGENZI MKUU

MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO